9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu

Queensland kuna aina mbalimbali ya mipango ya afya na huduma ambazo zinalenga na kuungamkono mahitaji maalum ya afya ya vikundu vya watu katika jamii. Huduma hizi hutolewa na serikali pamoja na mashirika yasiyo ya serikali. Mipango hiyo na huduma zimeorodheshwa hapa.

13HEALTH (**13 43 25 84**)

- kutoa ushauri unaoeleweka wa afya
- unaweza kupiga simu masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki kwa gharama ya kawaida ya simu
- uliza kama unahitaji mkalimani

Mpango wa Ruzuku ya Vifaa vya kusaidia walemavu

- huwapa wakazi wa Queensland wanaositahili wenye matatizo ya kiafya ya kudumu na wale wanaoendelea vizuri au ulemavu, uwezo wa kupata ruzuku kwa ajili ya vitu na vifaa vya kusaidia ulemavu mfano vifaa vya mawasiliano, vifaa vya kuzuia haja kubwa au ndogo, kusaidia kuishi, viyatu maalumu kwa ajili ya matibabu, vifaa vya kutembelea, matibabu ya mifupa na oksijeni.
- Kwa mawasiliano: Kituo cha Huduma cha MASS (07) **3250 8555**

Mpango wa Utoaji Miwani za macho

- Huwapatia wakazi wa Queensland wanaostahili aina mbalimbali za miwani ya macho walizo andikiwa na daktari bila ya malipo
- Maelezo zaidi: Laini ya 13 HEALTH, nambari ya simu **13 43 25 84**

Watoto na vijana

Mpango wa Huduma ya Msingi

- mpango kambambe wa afya kwa watoto wenye umri wa miaka 0-12
- Maelezo zaidi: Laini ya Afya ya Watoto (07) **3862 2333** au **1800 177 279** (nje Brisbane)

Kliniki za chanjo

- Kliniki za Afya ya Watoto, baadhi ya mabaraza vitongoji na madaktari wa familia hutoa chanjo za kinga kwa watoto wachanga na watoto bila malipo.
- Kwa maelezo zaidi: Laini ya Afya ya Watoto (07) **3862 2333** au **1800 177 279** (nje Brisbane)

Mpango wa afya ya usikivu

- watoto wote wanaozaliwa Queensland hufanyiwa majaribio ya kusikia. Ikiwa mtoto hatapita majaribio hayo atapewa rufaa ya kufuatilia maendeleo yake.
- Kwa mawasiliano : (07) **3131 6814** Msimamiaji wa Queensland

Huduma za Magonjwa ya akili kwa Watoto na Vijana

- ushauri wa bure, tathmini, matibabu na huduma ya watoto waliyo na umri wa miaka 0-18 wanaosumbuliwa na magonjwa ya akili hospitalini au katika huduma za jamii.
- Kwa maelezo zaidi: Kituo cha Tamaduni Mbalimbali cha Queensland cha Afya ya Akili (QLD transcultural health centre) (07) **3240 2833** au **1800 188189** (nje ya Brisbane)

Laini ya simu ya Kuwasaidia Watoto

- Watoto wanaweza kupiga simu **1800 551 800** kwa usaidizi na ushauri wa bure. Huduma inapatikana kwa masaa 24 kwa siku

Wanawake

Huduma za Uzazi

- Huduma ya kabla ya kujifungua huanzia na daktari wako wa familia ambaye atakupatia rufaa ya kwenda hospitali, kituo cha kujifungua au sehemu nyengine yoyote inayotoa huduma ya uzazi

Huduma ya Afya inayotembelea Wanawake

- ni mtandao wa huduma ya manesi 15 wenye mafunzo maalum ya afya za wanawake wanaofanya kazi katika maeneo ya mashambani na maeneo mengine ya Queensland yaliyo mbali
- Maelezo zaidi: Laini ya 13 HEALTH, nambari ya simu **13 43 25 84**

Kuchunguza Uvimbe katika Matiti Queensland

- hutoa huduma ya bure ya kuchunguza uvimbe katika matiti (kuchunguza tishu za matiti) kwa wanawake wenye umri wa miaka 40 na zaidi, haswa wanawake walio na umri wa miaka 50 hadi 69. Hii ni ili kugundua Kansa ya matiti
- Kwa mawasiliano: **13 20 50** kutoka mahali popote Queensland ili ufanye miadi

Upimaji mlango wa kizazi

- inapendekezwa kwamba wanawake ambao wanajihusisha na vitendo vya ngono wanapaswa kuanza kupimwa mlango wa kizazi (ili kugundua kansa ya mlango wa kizazi) kuanzia umri wa miaka 18 -20, au miaka miwili baada ya uhusikaji wa kufanya ngono kwa mara ya kwanza. Daktari wako au kliniki za jamii zinaweza kufanya upimaji huu.
- habari zaidi: Afya ya Wanawake Queensland Kote (07) **3839 9988** au **1800 017 676** (nje ya Brisbane) ili upate huduma iliyo karibu na wewe

Ugomvi wa Nyumbani na Ushambuliaji wa Kinjisia

- Wasiliana na: Huduma ya Msaada ya Wanawake Wahamiaji (Migrant Women Support Services) (07) **3846 5400** au (07) **3846 3490** kwa wakati wa mchana
- Mawasiliano: Laini ya Usaidizi ya Ushambulizi wa Kinjisia katika Queensland **1800 010 120** saa moja asubuhi hadi saa kumi na moja jioni

9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu

Huduma ya Afya ya Wanawake

- kuna huduma za afya ya wanawake za binafsi na zisizo za serikali katika Queensland
- Maelezo zaidi: Laini ya 13HEALTH (**13 43 25 84**)

Huduma za Magonjwa ya akili

- Tathmini ya bure, Matibabu na huduma kwa watu wazima waliyopitisha umri wa miaka 18 wanaosumbuliwa na magonjwa ya akili hospitalini au katika huduma za jamii
- Kwa maelezo zaidi: Kituo cha Tamaduni Mbalimbali cha Queensland cha Afya ya Akili (QLD transcultural health centre) (07) **3240 2833** au **1800 188189** (nje ya Brisbane)

Watu wazee

Huduma za Nyumbani na za Jamii (HACC)

- hutoa uwangalizi wa kawaida na huduma ya kusaidia wazee wasiojiweza (na vijan wenye ulemavu) ili waendelee kuishi katika jumuia zao.
- Kuna aina nyingi za huduma za nyumbani na za jamii (HACC), ikijumuisha huduma za lugha maalumu au vikundi vya kitamaduni.
- Wasiliana: Kitengo cha akiba ya maelezo 'resource unit' cha HACC cha Brisbane (07) **31394653**
- Wasiliana: Kituo cha 'Commonwealth Carelink' nambari ya simu **1800 052 222**

Huduma za wazee

- zinatolewa na serikali na mashirika ya siyo kuwa ya serikali katika nyumba nyumba za watu, vituo vya mapumziko na nyumba za kuuguza wazee
- huduma inajumuisha vyakula, usafiri, kazi za nyumbani, matembezi ya kijamii, huduma ya uuguzi, huduma nyingine zinazohusiana pamoja na mapumziko
- matunzo katika nyumba za kuuguza wazee hutolewa kwa wazee ambao wametathminiwa kuwa wanastahili matunzo ya hali ya juu, ambayo hayawezi kutolewa manyumbani kwao.
- Mawasiliano: Laini ya Habari ya Huduma ya Wazee **1800 500 853**

Kadi ya Wazee wa Queensland (Seniors Card)

- Wakazi wote wa Queensland waliyo na umri wa miaka 60 au zaidi wanastahiki Kadi ya Wazee au Kadi ya Kipunguzio ya Biashara ya wazee (Kadi ya discount) ambayo huwasaidia kupunguziwa bei kila mahali Queensland.
- Mawasiliano: Huduma Nadhifu ya Queensland **1800 175 500** au tembelea http://www.communities.qld.gov.au/seniorscard/

Msaada wa Walezi

- Maelezo na msaada kwa watu wanaowatunza wazee
- Mawasiliano: Laini ya Msaada na Maelezo ya Kituo cha 'Commonwealth Carer Resource Centre' **1800 242 636**

Huduma za afya ya kiakili

- Tathmini ya bure, Matibabu na Matunzo kwa watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanaosumbuliwa na magonjwa ya akili hospitalini au katika huduma za jamii
- Maelezo zaidi: Kituo cha Tamaduni Mbalimbali cha Queensland cha Afya ya Akili (QLD transcultural health centre) (07) **3240 2833** au **1800 188189** (nje ya Brisbane)

Wakimbizi

Kliniki za wakimbizi

- Kliniki ya Afya ya Jamii ya Wakimbizi (Brisbane) (07) **3480 2880**
- Mradi wa Afya ya Wakimbizi wa Logan (07) **33875370**

Usaidizi wa Mateso na Dhiki

- Mpango wa Queensland wa Kuwasaidia wakimbizi waliyonusurika na Mateso mbali mbali (07) **3391 6677**

Huduma za makazi (Husaidia na huduma kama zile za makazi, mapato, ajira, shule, uchukuzi, afya na darasa la Kiingereza)

- Shirika la Maendeleo la Tamaduni mbalimbali (07) **3337 5400** (Brisbane)
- Spiritus (07) **4639 3983** (Toowoomba)
- ACCESS (07) **3808 9299** Logan na Gold Coast
- Centacare Cairns (07) **4041 7699** (Cairns, Innisfail na vitongoji vyake)
- Kikundi cha Townsville cha Msaada wa Tamaduni mbalimbali (07) **4775 1588** (Townsville na vitongoji vyake)

Msaada wa wakimbizi wa kisiasa

- Wakimbizi ambao hawastahili Medicare wanapatiwa matibabu ya bure na Huduma za Afya za Queensland.
- Mawasiliano: Kituo cha Msaada wa Madai ya Wakimbizi (07) **3357 9013**

Huduma za afya ya kiakili

- Tathmini ya bure, Matibabu na Matunzo kwa watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanaosumbuliwa na magonjwa ya akili hospitalini au katika huduma za jamii
- Maelezo zaidi: Kituo cha Tamaduni Mbalimbali cha Queensland cha Afya ya Akili (QLD transcultural health centre) (07) **3240 2833** au **1800 188189** (nje ya Brisbane

Karatasi hii ya kweli iko katika mfululizo wa 10. idadi kamili:

1. Mfumo wa afya nchini Queensland
2. Kumwona daktari
3. Madawa
4. Hospitali za Queensland
5. Vituo vya afya ya jamii
6. Huduma za meno
7. Afya ya pamoja
8. Kuishi na afya na kuzuia magonjwa
9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu
10. Wewe na mfumo wa huduma ya afya

© QUEENSLAND HEALTH - JUNE 2007